**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# MWONGOZO WA VIKAO VYA KAMATI YA PAMOJA YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KATIKA MASUALA YA MUUNGANO

**Aprili, 2025**



*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (kushoto) na Sheikh Abeid Amani Karume wakibadilishana Hati za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 27 Aprili, 1964*

# YALIYOMO


**DIBAJI** ... iv

**SURA YA KWANZA** ... 1

**1.0 UTANGULIZI** ... 1

**1.1 Chimbuko la Mwongozo** ... 2

**1.2 Lengo la Mwongozo** ... 3

**1.2.1 Lengo Kuu** ... 3

**1.2.2 Malengo Mahsusi** ... 3

**SURA YA PILI** ... 4

**2.0 VIKAO VYA KAMATI YA PAMOJA YA SJMT NA SMZ KATIKA MASUALA YA MUUNGANO** ... 4

**2.1 KIKAO CHA KAMATI YA PAMOJA YA SJMT NA SMZ KATIKA MASUALA YA MUUNGANO** ... 4

**2.1.1 Wajumbe** ... 4

**2.1.2 Katibu** ... 5

**2.1.3 Majukumu** ... 6

**2.1.4 Uendeshaji wa Kikao cha Kamati ya Pamoja** ... 7

**2.2 KIKAO CHA MAWAZIRI WA SJMT NA SMZ** ... 7

**2.2.1 Wajumbe** ... 7

**2.2.2 Katibu** ... 8

**2.2.3 Majukumu** ... 9

**2.2.4 Uendeshaji wa Kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ** ... 9

**2.3 KIKAO CHA MAKATIBU WAKUU WA SJMT NA SMZ** ... 10

**2.3.1 Wajumbe** ... 10

**2.3.2 Katibu** ... 11

**2.3.3 Majukumu** ... 11

**2.3.4 Uendeshaji wa Kikao cha Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ** ... 12

**SURA YA TATU** ... 13

**3.0 VIKAO VYA KAMATI NDOGO ZA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA MUUNGANO** ... 13

**3.1 KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UCHUMI NA BIASHARA** ... 13

**3.1.1 Wajumbe** ... 13

**3.1.2 Katibu** ... 14

**3.1.3 Majukumu** ... 14

**3.1.4 Uendeshaji wa Vikao** ... 15

**3.2 KIKAO CHA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA** ... 16

**3.2.1 Wajumbe** ... 16

**3.2.2 Katibu** ... 17

**3.2.3 Majukumu** ........ 17
**3.2.4 Uendeshaji wa Vikao** ........ 18
**3.3 SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAMOJA YA SJMT NA SMZ KATIKA MASUALA YA MUUNGANO** ........ 18
**3.3.1 Wajumbe** ........ 18
**3.3.2 Katibu** ........ 19
**3.3.3 Majukumu** ........ 19
**3.3.4 Uendeshaji wa Kikao** ........ 20
**3.4 VIKAO VYA SEKTA** ........ 20
**3.4.1 Wajumbe** ........ 21
**3.4.2 Uendeshaji wa Vikao vya Sekta** ........ 22
**SURA YA NNE** ........ 24
**4.0 USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA VIKAO** ........ 24
**4.1 Uwasilishaji Hoja** ........ 24
**4.2 Uondoshaji wa Hoja** ........ 24
**4.3 Gharama za Vikao** ........ 25
**4.3.1 Vikao vya Kamati ya Pamoja** ........ 25
**4.3.2 Vikao vya Sekta** ........ 25
**4.4 Tathmini, Utekelezaji na Ufuatiliaji** ........ 25
**4.4.1 Ufuatiliaji** ........ 26
**4.4.2 Tathmini** ........ 26
**4.4.3 Utekelezaji** ........ 27
**4.5 Hitimisho** ........ 27

# DIBAJI



Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umeendelea kudumu kwa zaidi ya miaka 60 kutokana na dhamira ya dhati ya kuimarisha umoja na mshikamano wa kitaifa iliyoasisiwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Dhamira hii ilijikita katika kuunganisha nguvu za watu wa pande zote mbili ili kujenga taifa moja lenye usawa, amani, mshikamano na maendeleo ya pamoja. Mbali na dhamira ya waasisi, Muungano umeendelea kudumu kutokana na sababu nyingine muhimu, ikiwemo: Sera na misimamo ya pamoja kisiasa; Uongozi thabiti wa viongozi waliowafuata waasisi, ambao wameendeleza malengo ya Muungano kwa kujibu changamoto mpya zinazojitokeza kadiri jamii inavyokua; Mchango na uungwaji mkono wa wananchi, ambao wameendelea kuwa msingi wa uthabiti wa Muungano.

Aidha, uwepo wa mifumo imara ya majadiliano na utatuzi wa changamoto zinazoukabili Muungano, kama ilivyo kupitia Kamati ya Pamoja ya Serikali na vikao vya juu vya kikatiba, kumewezesha masuala mbalimbali kushughulikiwa kwa njia ya mazungumzo na maridhiano. Hii imeendelea kuimarisha uhusiano kati ya pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa pamoja, juhudi hizi zimewezesha Tanzania kupiga hatua kubwa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Muungano umeendelea kuwa kielelezo cha mafanikio katika bara la Afrika na kupata sifa kimataifa kama mfano wa kuigwa wa umoja, Amani na maendeleo endelevu.

Kipekee, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar

na Mwenyekiti wa wa Baraza la Mapinduzi, kwa jitihada zao kubwa na za makusudi katika kuhakikisha kuwa Muungano wetu unaendelea kudumishwa, kuimarishwa na kuleta manufaa makubwa kwa wananchi wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), kupitia Kamati ya Pamoja ya Kushughulikia Masuala ya Muungano iliyoanzishwa mwaka 2006, imeendelea kuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kupitia mfumo huu wa maridhiano na ushirikiano, pande zote mbili za Muungano zimekuwa zikijadiliana na kushughulikia masuala mbalimbali yanayojitokeza ili kuhakikisha maslahi ya wananchi yanazingatiwa. Vikao vya Kamati ya Pamoja hufanyika katika ngazi tofauti zinazojumuisha Wataalam, Makatibu Wakuu, Mawaziri pamoja na Kamati kuu ya Pamoja. Kupitia mchakato huu wa hatua kwa hatua, changamoto zote zinazohusiana na Muungano zimekuwa zikipewa majibu ya kudumu na kuendelea kuimarisha uhusiano wa kiutendaji kati ya SJMT na SMZ.

Mwaka 2019, SJMT na SMZ ziliandaa utaratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya kushughulikia masuala ya Muungano ili kuimarisha uratibu wa vikao hivyo. Mwaka 2025, utaratibu huo umepitiwa upya kwa lengo la la kuongeza ufanisi katika uratibu na ufuatiliaji wa maamuzi. Nina imani kuwa mwongozo huu mpya wa vikao vya Kamati ya Pamoja utatekelezwa kikamilifu na wote wanaohusika.

Dkt. Philip Isdor Mpango
**MAKAMU WA RAIS**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Muungano wa iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar uliasisiwa tarehe 26 Aprili, 1964. Aidha, Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, imeorodhesha Mambo 22 ya Muungano. Kwa mujibu wa Ibara ya 47 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Mambo ya Muungano. Katika kutekeleza jukumu hilo, kwa kuzingatia tangazo la Serikali la majukumu ya Wizara la mwezi Julai, 2021 Ofisi ya Makamu wa Rais imepewa jukumu la kuratibu masuala ya Muungano na kuratibu ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala Yasiyo ya Muungano.

Tangu kuasisiwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kumekuwa na mafanikio katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto katika kutekeleza Mambo ya Muungano. Kutokana na hali hiyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zimechukua hatua za kuhakikisha kuwa changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi. Hatua hizo ni pamoja na kuundwa kwa Tume na Kamati za kutatua changamoto hizo, kwa mfano Kamati ya Shellukindo ya mwaka 1992.

Mwaka 2006 Serikali iliendeleza jitihada hizo kwa kuanzisha vikao vya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jitihada hizo ziliendelea hadi mwezi Februari, 2008, ilipoundwa Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano (Kamati ya Pamoja) chini ya Uongozi na Uenyekiti wa Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania. Mwaka 2019 Utaratibu rasmi wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano uliandaliwa ili kuimarisha na kurasimisha utaratibu wa vikao vya Pamoja na kuweka muda kwa vikao vya kila ngazi. Katika kutekeleza Utaratibu huo, vikao vya kutafuta ufumbuzi wa hoja za Muungano viliweza kutatua na kuondoa hoja mbalimbali za Muungano zilizowasilishwa.

Hivyo, kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano kilichofanyika tarehe 6 Machi, 2024 Zanzibar kilitoa maelekezo ya kufanya mapitio ya Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano wa mwaka 2019. Kufuatia maelekezo hayo, Ofisi imeandaa Mwongozo wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ katika Masuala ya Muungano wa mwaka 2025.

Jitihada zote hizi zinafanyika kwa lengo la kuhakikisha kuwa, Serikali zetu mbili zinakutana, kujadiliana na kuzitafutia ufumbuzi hoja mbalimbali zinazoibuliwa ili kuondoa malalamiko kwa Watanzania. Hatua hii itawafanya Wananchi kuendelea kuuthamini, kuuenzi na kuulinda Muungano huu.

Kwa muktadha huo, ni wazi kuwa Mwongozo huu utaimarisha utekelezaji wa majukumu ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kusimamia utekelezaji wa Mambo ya Muungano kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

## 1.1 Chimbuko la Mwongozo

Chimbuko la Mwongozo huu ni Agizo la Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano kilichofanyika Zanzibar, tarehe 13 Januari, 2017 ili kuwa na uratibu na ufuatiliaji wenye tija wa makubaliano yaliyofikiwa na pande mbili na kuhakikisha vikao vya Kamati ya

Pamoja vinafanyika kwa wakati na utekelezaji wa maamuzi unaboreshwa.

## 1.2 Lengo la Mwongozo

### 1.2.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la Mwongozo huu ni kuweka utaratibu maalum wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ katika Masuala ya Muungano.

### 1.2.2 Malengo Mahsusi

a) Kurasimisha uratibu wa vikao vya Muungano.

b) Kutoa uelewa wa pamoja wa vikao vya utatuzi wa changamoto za Muungano na masuala mengine yenye maslahi mapana ya pande mbili za Muungano ikiwemo fursa zilizopo.

c) Kuwezesha vikao kufanyika kwa wakati.

# SURA YA PILI

## 2.0 VIKAO VYA KAMATI YA PAMOJA YA SJMT NA SMZ KATIKA MASUALA YA MUUNGANO

Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ katika Masuala ya Muungano ni Kamati maalum ya Kitaifa ya pande mbili za Muungano inayoongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati hii hutoa maelekezo katika masuala yanayohusu Muungano kupitia mtiririko wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ.

Vikao vya Kamati ya Pamoja vitakuwa kwenye ngazi tatu ambazo ni:

a) Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ katika Masuala ya Muungano;

b) Kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ; na

c) Kikao cha Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ.

Vikao vyote vitaratibiwa na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ katika Masuala ya Muungano.

## 2.1 KIKAO CHA KAMATI YA PAMOJA YA SJMT NA SMZ KATIKA MASUALA YA MUUNGANO

Hiki ni kikao cha ngazi ya juu kabisa katika mtiririko wa vikao vya Kamati ya Pamoja.

### 2.1.1 Wajumbe

Kikao hiki kitahusisha wajumbe wafuatao:

a) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mwenyekiti;

b) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mjumbe;

c) Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar - Mjumbe;

d) Mawaziri wote – SJMT - Wajumbe;

e) Mawaziri wote – SMZ - Wajumbe;

f) Mwanasheria Mkuu wa Serikali – SJMT - Mjumbe;

g) Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar – SMZ – Mjumbe;

h) Katibu Mkuu Kiongozi – SJMT – Mjumbe;

i) Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi – SMZ – Mjumbe;

j) Makatibu Wakuu wote - SJMT - Wajumbe;

k) Makatibu Wakuu wote – SMZ - Wajumbe;

l) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali – SJMT - Mjumbe; na

m) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar – SMZ – Mjumbe.

### 2.1.2 Katibu

Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Muungano (SJMT) atakuwa Katibu wa Kikao hiki akishirikiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ).

Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja inaweza kushauri kualikwa kwa washiriki wengine itakapoonekana inafaa.

Kutokana na umuhimu wa kusimamia utekelezaji wa maagizo ya Kikao cha Kamati ya Pamoja kwa Serikali za pande mbili za Muungano, endapo Waziri Mkuu au Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar atashindwa kuhudhuria kikao cha Kamati ya Pamoja, atateuliwa Waziri mwandamizi kutoka Serikali husika kukaimu nafasi ya Waziri Mkuu au Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

### 2.1.3 Majukumu

Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ katika Masuala ya Muungano, kitakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kupokea taarifa za utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa katika Kikao cha Kamati ya Pamoja;

b) Kutoa uamuzi wa makubaliano yaliyofikiwa katika kikao cha Mawaziri;

c) Kutoa maelekezo na maagizo kwa hoja ambazo hazijapatiwa ufumbuzi;

d) Kuidhinisha hoja mpya na kuzitolea maelekezo;

e) Kutoa maelekezo kwa masuala yoyote yatakayokua na maslahi katika Muungano; na

f) Kupokea na kujadili masuala mengine yenye maslahi mapana kwa pande mbili ikiwemo fursa mbalimbali zinazopatikana ndani na nje ya nchi kwa maslahi ya pande mbili za Muungano.

### 2.1.4 Uendeshaji wa Kikao cha Kamati ya Pamoja

Kikao cha Kamati ya Pamoja kitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:

a) Kikao kitafanyika mwezi wa Aprili ya kila mwaka na Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao maalum itakapohitajika;

b) Uamuzi wa kikao utafanywa na Mwenyekiti baada ya kushauriana na Waziri Mkuu wa SJMT na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar au Waziri atakayekaimu nafasi ya Waziri Mkuu wa SJMT au Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar; na

c) Kikao kitafanyika pande zote mbili za Muungano kwa mzunguko. Hata hivyo, kinaweza kufanyika upande mmoja mfululizo kwa makubaliano ya pande mbili za Muungano.

## 2.2 KIKAO CHA MAWAZIRI WA SJMT NA SMZ

Kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ kitakua kikao cha ngazi ya pili katika mtiririko wa vikao vya Kamati ya Pamoja.

Vikao hivi vitaongozwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) au Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar (SMZ). Kikao kikifanyika Tanzania Bara, Mwenyekiti wa kikao atatoka SJMT na Mwenyekiti Mwenza atatoka SMZ au kinyume chake.

### 2.2.1 Wajumbe

Wajumbe wa kikao hiki watakuwa ni:

a) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania -– Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza;

b) Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar - Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza;

c) Mawaziri wote wa SJMT - Wajumbe;

d) Mawaziri wote wa SMZ - Wajumbe;

e) Mwanasheria Mkuu wa Serikali – SJMT - Mjumbe;

f) Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar – SMZ - Mjumbe;

g) Katibu Mkuu Kiongozi wa SJMT - Mjumbe;

h) Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi– SMZ - Mjumbe;

i) Makatibu Wakuu wote – SJMT - Wajumbe;

j) Makatibu Wakuu wote – SMZ – Wajumbe;

k) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali – SJMT - Mjumbe; na

l) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar – SMZ – Mjumbe.

### 2.2.2 Katibu

Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais – SJMT na Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – SMZ - watakuwa Katibu au Katibu mwenza wa kikao hiki kulingana na upande kinapofanyika kikao.

Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja inaweza kushauri kualikwa kwa washiriki wengine itakapoonekana inafaa.

### 2.2.3 Majukumu

Kikao hiki kitakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kupokea taarifa za utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa katika kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ;

b) Kutoa uamuzi kwa makubaliano yaliyofikiwa katika kikao cha Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ;
c) Kutoa maelekezo na maagizo kwa Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ juu ya hoja ambazo hazijapatiwa ufumbuzi;

d) Kutekeleza maagizo ya kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ katika Masuala ya Muungano;

e) Kutoa ushauri kwa Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ katika Masuala ya Muungano;

f) Kupokea na kupitisha hoja mpya; na

g) Kupokea taarifa ya fursa mbalimbali zinazopatikana ndani na nje ya nchi kwa maslahi ya pande mbili za Muungano.

### 2.2.4 Uendeshaji wa Kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ

Kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ kitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:

a) Kikao kitafanyika mwezi Aprili ya kila mwaka na endapo kutakuwa na uhitaji mahsusi, kikao maalum kitaitishwa;

b) Uamuzi wa kufanya kikao utafanywa na Mwenyekiti baada ya kushauriana na Mwenyekiti Mwenza; na

c) Kikao kitafanyika pande zote mbili za Muungano kwa mzunguko. Hata hivyo, kinaweza kufanyika upande mmoja mfululizo kwa makubaliano.

## 2.3 KIKAO CHA MAKATIBU WAKUU WA SJMT NA SMZ

Kikao cha Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ kitakua kikao cha ngazi ya tatu katika mtiririko wa vikao vya Kamati ya Pamoja.

Iwapo Mwenyekiti atapata dharura itakayosababisha kutoweza kuongoza kikao, atalazimika kufanya mawasiliano na Mwenyekiti Mwenza ili kikao kifanyike.

### 2.3.1 Wajumbe

Wajumbe wa kikao hiki ni:

a) Katibu Mkuu Kiongozi wa SJMT – Mwenyekiti/ Mwenyekiti Mwenza

b) Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi - Mwenyekiti / Mwenyekiti Mwenza;

c) Makatibu Wakuu wote – SJMT – Wajumbe;

d) Makatibu Wakuu wote – SMZ - Wajumbe;

e) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali - SJMT - Mjumbe; na

f) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar - SMZ – Mjumbe.

### 2.3.2 Katibu

a) Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais SJMT - Katibu/ Katibu Mwenza; na

b) Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais SMZ - Katibu/Katibu Mwenza.

Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja inaweza kushauri kualikwa kwa washiriki wengine itakapoonekana inafaa.

### 2.3.3 Majukumu

Kikao hiki kitakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kutekeleza maagizo yaliyotolewa katika kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ na kuwasilisha taarifa;

b) Kupokea taarifa za utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa katika kikao cha Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ;

c) Kutoa uamuzi wa makubaliano yaliyofikiwa katika vikao vya kisekta;

d) Kutoa maagizo kwa sekta husika za SJMT na SMZ;

e) Kutoa ushauri kwa Mawaziri wa SJMT na SMZ kuhusu utekelezaji wa masuala ya Muungano;

f) Kupokea, kujadili na kuwasilisha hoja mpya katika kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ; na

g) Kujadili na kutoa ushauri kuhusu fursa mbalimbali zinazopatikana ndani na nje ya nchi kwa maslahi ya pande mbili za Muungano.

### 2.3.4 Uendeshaji wa Kikao cha Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ

Kikao cha Makatibu wa Wakuu wa SJMT na SMZ kitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:

a) Kikao kitafanyika mara mbili kwa mwaka ambapo kikao cha kwanza kitafanyika mwezi Aprili ya kila mwaka na kikao cha pili kitapangwa kufanyika kutokana na mahitaji ya wakati husika. Aidha, kikao maalum kinaweza kuitishwa;

b) Uamuzi wa kikao utafanywa na Mwenyekiti baada ya kushauriana na Mwenyekiti Mwenza;

c) Kikao kitafanyika pande zote mbili za Muungano kwa mzunguko. Hata hivyo, kinaweza kufanyika upande mmoja mfululizo kwa makubaliano; na

d) Iwapo kikao kitafanyika Tanzania Bara, Katibu Mkuu Kiongozi (SJMT) ndiye atakuwa Mwenyekiti wa kikao na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi (SMZ) atakuwa Mwenyekiti Mwenza au kinyume chake.

## SURA YA TATU

## 3.0 VIKAO VYA KAMATI NDOGO ZA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA MUUNGANO

Kutakuwa na vikao vya Kamati ndogo mbili, ambazo ni: Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara; na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kamati hizi zitakuwa na jukumu la kuzipatia ufumbuzi changamoto zozote zinazotokana na Utekelezaji wa majukumu ya Kisekta miongoni mwa Mambo 22 ya Muungano. Aidha, Changamoto hizo zitakuwa zinawasilishwa katika vikao hivyo ili kupatiwa utatuzi wa haraka badala ya kusubiri utaratibu wa kawaida wa Vikao vya Kamati ya Pamoja vya SJMT na SMZ. Kamati hizi zitawasilisha taarifa ya utekelezaji katika Vikao vya Kamati ya Pamoja vya SJMT na SMZ. Aidha, vikao hivi vitaratibiwa na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ katika Masuala ya Muungano.

## 3.1 KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UCHUMI NA BIASHARA

### 3.1.1 Wajumbe

Wajumbe wa Kamati hii ni:

a) Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Muungano, SJMT– Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza;

b) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, SMZ - Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza;

c) Mawaziri wenye dhamana na masuala ya Fedha na Mipango, SJMT na SMZ - Wajumbe

d) Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya Biashara na Viwanda, SJMT na SMZ - Wajumbe;

e) Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya Uchukuzi, SJMT na SMZ – Wajumbe;

f) Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya Uwekezaji, SJMT na SMZ - Wajumbe;

g) Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania – Mjumbe;

h) Makatibu Wakuu wenye dhamana ya masuala ya Viwanda na Biashara, SJMT na SMZ - Wajumbe;

i) Makatibu Wakuu wenye dhamana ya masuala ya Fedha na Mipango, SJMT na SMZ - Wajumbe; na

j) Makatibu Wakuu wa Uchukuzi, SJMT na SMZ – Wajumbe.

Sekretarieti inaweza kumwalika mjumbe mwingine kadri itakavyoonekana inafaa.

### 3.1.2 Katibu

a) Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais SJMT - Katibu/ Katibu Mwenza; na

b) Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais SMZ - Katibu/Katibu Mwenza.

### 3.1.3 Majukumu

Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara itakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kujadili na kubuni mbinu za kutatua changamoto zinazohitaji ufumbuzi wa haraka kwa sekta husika;

b) Kutoa taarifa za utekelezaji wa changamoto zilizopatiwa ufumbuzi kwa Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ;

c) Kuwasilisha taarifa ya hoja zinazohitaji maamuzi kwa Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ;

d) Kuwasilisha taarifa za hatua za utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa katika vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ kwa kila robo mwaka wa fedha; na

e) Kujadili na kutoa ushauri kuhusu fursa mbalimbali zinazopatikana ndani na nje ya nchi kwa maslahi ya pande mbili za Muungano.

### 3.1.4 Uendeshaji wa Vikao

Vikao vya Kamati hii vitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:

a) Vikao vitafanyika katika robo ya tatu au ya nne ya kila mwaka wa fedha na muda wowote itakapotokeza haja ya kukutana;

b) Uamuzi wa vikao utafanywa na Mwenyekiti baada ya makubaliano ya Wajumbe; na

c) Vikao vitafanyika pande zote mbili za Muungano kwa kupokezana. Hata hivyo, vinaweza kufanyika upande mmoja mfululizo kwa makubaliano.

## 3.2 KIKAO CHA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA

### 3.2.1 Wajumbe

Wajumbe wa Kamati hii ni:

a) Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Muungano, SJMT na SMZ – Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza;

b) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, SMZ – Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza;

c) Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya Katiba na Sheria, SJMT na SMZ – Wajumbe;

d) Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya ushirikiano wa Kimataifa, SJMT na SMZ- Wajumbe;

e) Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya Sera na Uratibu SJMT na SMZ – Wajumbe;

f) Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, SJMT na SMZ – Wajumbe;

g) Mwanasheria Mkuu wa Serikali, SJMT – Mjumbe;

h) Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, SMZ – Mjumbe;

i) Makatibu Wakuu wenye dhamana ya masuala ya Katiba na Sheria, SJMT na SMZ – Wajumbe; na

j) Makatibu Wakuu wenye dhamana ya masuala ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, SJMT na SMZ – Wajumbe.

Sekretarieti inaweza kumwalika mjumbe mwingine kadri itakavyoonekana inafaa.

### 3.2.2 Katibu

a) Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais SJMT - Katibu/ Katibu Mwenza; na

b) Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais SMZ - Katibu/Katibu Mwenza.

### 3.2.3 Majukumu

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala itakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kujadili na kubuni mbinu za kutatua changamoto zinazohitaji ufumbuzi wa haraka kwa sekta husika;

b) Kutoa taarifa za utekelezaji wa changamoto zilizopatiwa ufumbuzi kwa Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ;

c) Kuwasilisha taarifa ya hoja zinazohitaji maamuzi kwa Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ;

f) Kuwasilisha taarifa za hatua za utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa katika vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ kwa kila robo mwaka wa fedha; na

d) Kujadili na kutoa ushauri kuhusu fursa mbalimbali zinazopatikana ndani na nje ya nchi kwa maslahi ya pande mbili za Muungano.

### 3.2.4 Uendeshaji wa Vikao

Vikao vya Kamati hii vitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:

a) Vikao vitafanyika katika robo ya tatu au ya nne ya kila mwaka wa fedha na muda wowote itakapotokeza haja ya kukutana;

b) Uamuzi wa vikao utafanywa na Mwenyekiti baada ya makubaliano ya Wajumbe; na

c) Vikao vitafanyika pande zote mbili za Muungano kwa kupokezana. Hata hivyo, vinaweza kufanyika upande mmoja mfululizo kwa makubaliano.

## 3.3 SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAMOJA YA SJMT NA SMZ KATIKA MASUALA YA MUUNGANO

### 3.3.1 Wajumbe

Kutakuwa na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ katika Masuala ya Muungano ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

a) Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais - SJMT - Mwenyekiti/ Mwenyekiti Mwenza;

b) Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - SMZ - Mwenyekiti/Mwenyekiti Mwenza;

c) Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – SJMT - Mjumbe;

d) Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria, SJMT – Mjumbe;

e) Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu, SMZ – Mjumbe;

f) Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora – SMZ – Mjumbe; na

g) Naibu Katibu Mkuu anayesimamia masuala ya Muungano wa SJMT na SMZ – Mjumbe.

Mwenyekiti anaweza kushauri kualikwa kwa washiriki wengine inapoonekana inafaa.

### 3.3.2 Katibu

a) Mkurugenzi wa Idara ya Muungano –SJMT – Katibu/Katibu Mwenza; na

b) Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali – SMZ – Katibu/Katibu Mwenza.

### 3.3.3 Majukumu

Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja itakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kuratibu vikao vya ngazi zote za Kamati ya Pamoja;

b) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya vikao na kuandaa taarifa;

c) Kutoa ushauri kwa ngazi zote za Kamati ya Pamoja;

d) Kutunza kumbukumbu za vikao vya ngazi zote;

e) Kuandaa ratiba ya vikao vinavyohusu masuala ya Muungano na kuiwasilisha kwa viongozi; na

f) Kufanya kazi zote itakazopangiwa na Kamati ya Pamoja.

### 3.3.4 Uendeshaji wa Kikao

Kikao hiki kitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:

a) Kikao kitafanyika mara nne kwa mwaka na kutokana na mahitaji kikao maalum kinaweza kuitishwa;

b) Uamuzi wa kikao utafanywa na Mwenyekiti baada ya makubaliano ya Wajumbe wa Sekretarieti;

c) Kikao kitafanyika pande zote mbili za Muungano kwa mzunguko. Hata hivyo, kinaweza kufanyika upande mmoja mfululizo kwa makubaliano; na

d) Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais zitaandaa ratiba ya mwaka ya vikao vya sekta na kusambaza kwa sekta husika mwezi Julai ya kila mwaka.

## 3.4 VIKAO VYA SEKTA

Kutakuwa na vikao vya sekta ambavyo vitaratibiwa na kusimamiwa na Sekta husika za SJMT na SMZ. Vikao hivyo, vitaitishwa kwa kuzikutanisha sekta zenye hoja. Lengo la vikao hivi ni kuziwezesha sekta husika kuwa na uelewa wa pamoja juu ya hoja au fursa iliyopo na kuangalia namna bora ya kutafuta ufumbuzi na kushauri ipasavyo kwa ngazi zinazofuata.

### 3.4.1 Wajumbe

Wajumbe wa vikao hivi ni:

**a) Ngazi ya Mawaziri**

**Wajumbe**

i) Mawaziri wenye dhamana ya sekta husika, SJMT na SMZ – Mwenyekiti/Mwenyekiti mwenza;

ii) Makatibu Wakuu wa sekta husika SJMT na SMZ – Wajumbe; na

iii) Mwakilishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Wajumbe

**Katibu**

i) Katibu Mkuu, Sekta husika (SJMT) – Katibu/Katibu mwenza; na

ii) Katibu Mkuu, Sekta husika (SMZ) – Katibu/Katibu Mwenza.

**b) Ngazi ya Makatibu Wakuu**

**Wajumbe**

i) Makatibu Wakuu wenye dhamana na Sekta husika SJMT na SMZ – Mwenyekiti/Mwenyekiti mwenza;

ii) Wakurugenzi wa Idara wa sekta husika, SJMT na SMZ – Wajumbe; na

i) Mwakilishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Wajumbe.

**Katibu**

i) Mkurugenzi wa Sekta husika (SJMT) - Katibu/Katibu mwenza; na

ii) Mkurugenzi wa Sekta husika (SMZ) - Katibu/Katibu mwenza.

**c) Ngazi ya Wataalamu**

i) Mkurugenzi wa Sekta husika, SJMT na SMZ – Mwenyekiti/Mwenyekiti mwenza.

ii) Mwakilishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Wajumbe

**Katibu**

Wakurugenzi Wasaidizi/Naibu Mkurugenzi/Wakuu wa Divisheni wa Sekta husika – Katibu/Katibu mwenza

### 3.4.2 Uendeshaji wa Vikao vya Sekta

Vikao vya sekta vitaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:

a) Vikao hivi vitaitishwa wakati wowote kulingana na mahitaji na kwa kuzingatia maelekezo;

b) Sekta zitashauriana na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ katika maandalizi na utaratibu wa uendeshaji wa vikao hivi ikihusisha gharama za kikao na taratibu nyingine; na

c) Sekta zitaandaa taarifa ya pamoja chini ya Uratibu wa Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja kwa ajili ya kuwasilisha katika ngazi husika.

**TANBIHI:** Vikao hivi vitaitishwa na kuratibiwa na sekta husika ambapo watapaswa kutoa taarifa kwa Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

## SURA YA NNE

# 4.0 USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA VIKAO

## 4.1 Uwasilishaji Hoja

Hoja za Muungano ni vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano yanayohusu maendeleo ya Wananchi katika Nyanja za kiuchumi na kijamii ambayo hupelekea vikwazo au kutotekelezwa vyema kwa mipango ya Wananchi na Serikali katika pande mbili za Muungano.

Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais zitapokea hoja zinazoleta changamoto katika utekelezaji wa masuala ya Muungano kutoka katika Wizara za Muungano na zisizo za Muungano.

Hoja zitakazowasilishwa ni zile zilizoshindwa kupatiwa ufumbuzi baada ya kufanyika kwa vikao vya wataalamu, Makatibu Wakuu na ngazi ya Mawaziri. Hoja kutoka katika Wizara za Muungano na zisizo za Muungano zitatakiwa kuwasilishwa mapema kwenye Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ili kutoa fursa ya kutosha kujadiliwa katika ngazi zote za vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ.

## 4.2 Uondoshaji wa Hoja

Hoja zote zinazojadiliwa zitapatiwa ufumbuzi katika Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ambacho ni kikao cha ngazi ya juu kinachotoa maamuzi ya pande zote mbili za Muungano.

Baada ya hoja kupatiwa ufumbuzi, kutaandaliwa maandishi ya uthibitisho (Hati) wa kumalizika kwa hoja hizo na kusainiwa na

Mawaziri wa Sekta husika na kushuhudiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.

## 4.3 Gharama za Vikao

### 4.3.1 Vikao vya Kamati ya Pamoja

Vikao vya Kamati ya Pamoja katika ngazi zote vitagharamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Gharama hizo zitakuwa ni ukumbi, chakula, shajala na posho za vikao kwa wajumbe. Posho hizo zitalipwa kulingana na utaratibu wa ulipaji wa vikao vya Serikali. Aidha, kuhusu posho ya kujikimu wajumbe pamoja na washiriki wote wa vikao hivi watagharamiwa na Taasisi zao.

Wizara zitakuwa na jukumu la kuwapokea viongozi wa Wizara zinazoshabihiana kimajukumu kwa kuwapatia huduma ya usafiri (gari, mafuta na dereva) kwa kipindi chote watakachokuwepo kwa ajili ya vikao isipokuwa kwa Viongozi Wakuu. Utaratibu huu utatumika katika vikao vya Kamati ya Pamoja na hivyo utasaidia kukuza ushirikiano baina ya viongozi wa pande mbili na Serikali kwa ujumla.

### 4.3.2 Vikao vya Sekta

Bajeti ya kikao (Ukumbi, Chakula na Shajala) itagharamiwa na upande ulioandaa kikao, na vikao hivi vitafanyika kila upande wa Muungano kwa kubalishana.

## 4.4 Tathmini, Utekelezaji na Ufuatiliaji

Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Pamoja ili kuhakikisha utekelezaji unafanyika ipasavyo. Baada ya kikao

cha Kamati ya Pamoja, Wizara au Sekta zilizopewa maagizo zitatakiwa kutekeleza maagizo na maelekezo kwa wakati uliopangwa, na endapo kutakuwa na changamoto katika utekelezaji wa maagizo watatakiwa kutoa taarifa kwenye Kamati ya Pamoja ili maelekezo zaidi yatolewe. Aidha, Wizara zenye maagizo zinatakiwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maagizo hayo Ofisi ya Makamu wa Rais, SJMT na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, SMZ katika kipindi kilichotolewa kwa ajili ya hatua zaidi. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo hayo utazingatia mambo yafuatayo:

### 4.4.1 Ufuatiliaji

a) Kufuatilia utekelezaji wa hoja zilizopatiwa ufumbuzi na kuandaliwa hati.
b) Ufuatiliaji wa vikao vya masuala ya Muungano kwa ajili ya kuimarisha shughuli za vikao hivyo.
c) Ufuatiliaji wa maagizo yaliyotolewa katika vikao vya Kamati ya Pamoja.
d) Utoaji wa taarifa mbalimbali za uendeshaji na utendaji wa vikao.

### 4.4.2 Tathmini

Tathmini ya mwongozo italenga kuona kama vikao vimesaidia kubadilisha, kuondosha na kupunguza hoja za Muungano. Aidha, tathmini itaongeza wigo, ubora na ufanisi wa vikao na shughuli zilizofanyika. Tathmini hii itafanyika kila mwaka na itaangalia viashiria vifuatavyo:

a) Idadi ya vikao vilivyofanyika;
b) Idadi ya hoja zilizotatuliwa/kupatiwa ufumbuzi; na
c) Idadi ya hoja zinazofanyiwa kazi.

Ufuatiliaji na tathmini uzingatie utekelezaji wa kila kikao kama ilivyoainishwa katika mwongozo huu. Ufuatiliaji na tathmini utaonesha vigezo vya ubora na taarifa za mwaka. Masuala mengine yatakayozingatiwa ni mtiririko wa uandaaji na uwasilishaji wa taarifa.

### 4.4.3 Utekelezaji

Sekretarieti ya vikao vya Muungano itakuwa na dhamana ya kufanya utekelezaji wa shughuli za vikao. Utekelezaji wa mwongozo huu utazingatia mambo yafuatayo:

a) Kuziandikia barua Wizara ama Taasisi zilizopatiwa maelekezo ya kuzifanyia kazi hoja za masuala ya Muungano; na
b) Kuziandikia barua Wizara na Taasisi kuzipatia taarifa za vikao vya masuala ya Muungano

## 4.5 Hitimisho

Serikali zote mbili zina nia thabiti ya kuondosha mambo yote yanayoleta vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Hivyo, ufanisi wa vikao hivi utasaidia kupunguza au kuondoa changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano hatimaye kuimarisha Muungano kwa manufaa ya pande mbili za Muungano. Pia, vikao hivi vinatoa fursa kwa Wizara, Idara na Taasisi za pande zote za Muungano kubadilishana uzoefu na jinsi ya kukabiliana na changamoto mbalimbali kwa manufaa ya wananchi kwa ujumla.



*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume wakisaini Hati za Makubaliano ya Muungano, Tarehe 22 Aprili, 1964 mjini Zanzibar. Wanaoshuhudia kwa karibu tukio hilo kushoto kwa Mwalimu ni Abdullah Kassim Hanga na kulia ni Oscar Kambona.*



*Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akichanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar huku akishuhudiwa na Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Zanzibar na Makamu wa Kwanza wa Rais, na Mhe. Rashidi Mfaume Kawawa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa sherehe za Muungano tarehe 26 Aprili, 1965. Walioshika chungu ni Bw. Hassan Omari Mzee (kulia) na Bw. Hasanaeli Elisaeli Mrema (kushoto).*



*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika na Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar Picha ya pamoja na viongozi mbalimbaili katika Ukumbi wa Karimjee - Dar es Salaam tarehe 27 Aprili, 1964.*